

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA TISA WA MWAKA

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa Wanahisa wa Maendeleo Bank PLC utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 24 Juni 2023 katika ukumbi wa Msasani, Dar es Salaam kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mkutano utatanguliwa na semina inayohusu Majukumu ya Wanahisa katika ukuaji endelevu wa benki na kufanikisha matarajiyo ya Wawekezaji: Uzoefu wa miaka 10 ya Maendeleo Bank.

Ajenda za Mkutano ni:

1. Kufungua Mkutano
2. Kupokea na Kupitisha Ajenda za Mkutano Mkuu wa 9 wa Mwaka 3. Kupitia na Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 8 wa Mwaka.
4. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa 8 wa Mwaka
5. Taarifa ya Wakurugenzi kwa Mwaka Ulioishia tarehe 31 Disemba 2022
6. Taarifa ya Mkaguzi wa Nje na Taarifa za Fedha Zilizokaguliwa kwa Mwaka Ulioishia tarehe 31 Disemba 2022
7. Kupokea na Kuidhinisha mapendekezo ya Posho na Ada za Wakurugenzi kwa Mwaka 2023
8. Kupokea na Kuidhinisha Mapendekezo ya Mkaguzi wa Nje kwa Mwaka Utakaoishia Tarehe 31 Disemba 2023
9. Kupokea na Kuidhinisha Pendekezo la Gawio
10. Uteuzi wa Wakurugenzi wa Bodi
11. Mengineyo
12. Kupanga Tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka Ujao

ZINGATIO:

1. Mwanahisa anayetaka kuhudhuria mkutano atajigharamia mwenyewe na anapaswa kuja kwenye mkutano akiwa na cheti cha Hisa/ Taarifa ya Akaunti inayotolewa na Soko la Hisa (DSE) na kitambulisho chenye picha kwa ajili ya utambulisho.
2. Mkutano pia utafanyika kwa njia ya mtandao wa zoom anuani ya mkutano itatumwa kwenye barua pepe au namba ya simu ya Mwanahisa iliyosajiliwa Benki. Hivyo wanahisa wanaopendelea kuhudhuria mkutano huu kwa njia ya mtandao wa zoom, wawasiliane na Katibu wa Benki kupitia barua pepe: shareholders@maendeleobank.co.tz au ujumbe wa simu / WhatsApp kupitia +255677 500050 hadi 23 Juni 2023 ili kupata taarifa na muongozo wa namna ya kushiriki kwenye mkutano huu.
3. Nakala za vitabu vya Mkutano Mkuu na fomu za uwakilishi zitapatikana Makao Makuu ya Maendeleo Bank, yaliyopo Luther House, Barabara ya Sokoine, kuanzia tarehe 15 Juni, 2023, na pia vitabu vitapatikana ukumbini hiyo tarehe 24 Juni 2023.
4. Mwanahisa anayestahili kuhudhuria Mkutano na ambaye ataona kwamba hataweza kuhudhuria yeye mwenyewe, anatakiwa kumteua Mwakilishi wake kwa kujaza fomu za uwakilishi na kuziwasilisha zikiwa zimetwa saini na kubandikwa stempu za ushuru za TZS 500 na zifikishwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Maendeleo Bank PLC, saa 48 kabla ya tarehe ya Mkutano. Ikiwa Mwanahisa ni kampuni, fomu ya mwakilishi lazima iwe na lakiri ya kampuni na aje akiwa na cheti cha Hisa.
5. Mapendekezo yoyote ya Wanahisa yapelekwe/yatumwe kwa Katibu kupitia barua pepe shareholders@maendeleobank.co.tz au WhatsApp namba +255677500050 saa 48 kabla ya tarehe ya Mkutano.



**KWA AGIZO LA BODI
IBRAHIM MWANGALABA 24 MEI 2023**